Al-Islam.org
Ahlul Bayt Digital Islamic Library Project
Published on *Al-Islam.org* (https://www.al-islam.org)



# Ulimi na Maovu Yake

369. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.,** *Bihar al-Anwaar, J. 71, Uk.286:*

*"Matokeo yatokanayo na ulimi ni mabaya kabisa, kuliko dharuba ya upanga mkali!"*

370. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.** *Bihar al-Anwaar J. 71 Uk.277:*

*"Miongoni mwa mambo yote, ulimi unastahili kuwekwa katika mahabusu kwa kipindi kirefu zaidi kuliko kitu kingine chochote.* (*Kwa sababu madhambi yetu mengi yana tokana nayo, kama vile kuwasuta watu, kusema uongo, kuzua mambo, kuwadhihaki wengine, na vile vile kuwa tuhumu watu wengi, n.k*)

371. **Amesema Al Imam Amiril Momineen a.s.** *Ghurar-ul-Hikam Uk. 228:*

*"Fikirieni na mupime kabla hamja ongea ili kwamba muweze kujizuia dhidi ya* (*kutenda*) *makosa."*

372. **Amesema Mtume Muhammad Mustafa s.a.w.w.** *Waqayi-ul-Ayyam, Uk. 297:*

*"Maangamizo ya mtu yako katika mambo matatu "Tumbo lake, matamaniyo yake, na ulimi wake."*

373. **Amesema Al Imam Muhammad al-Baqir a.s.** *Bihar al-Anwaar, J. 78, Uk.178:*

*"Hakuna mtu yeyote aliye salimika kutokana na ulimi wake hadi hapo yeye atakapo udhibiti ulimi wake."*

**Source URL:**
https://www.al-islam.org/sw/hadith-za-mtume-s-na-ma-imamu-1-700-amiraly-m-h-datoo/ulimi-na-maovu-yake#comment-0